



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA



*Unapojibu tafadhali taja:*

Kumb. Na. HMD/S.20/39/33

26 Mei, 2022

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma anapenda kuwatangazia waombaji wenye sifa kujaza nafasi za kazi katika kada zifuatazo:-

### 1.0 KATIBU MAHSUSI DARAJA LA III - NAFASI TATU (03)

#### 1.1 SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa wenye Elimu ya Kidato cha Nne (IV) au Sita (VI) aliyehitimu mafunzo ya Uhazili na kufaulu mtihani wa Hatua ya Tatu. Awe amefaulu somo la Hatimkato ya Kiswahili na Kiingereza maneno 80 kwa dakika moja na awe amepata mafunzo ya Kompyuta kutoka chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali na kupata cheti katika program za *Windows, Microsoft Office, Internet, Email na Publisher.*

#### 1.2 MAJUKUMU YA KAZI:

- (i) Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida
- (ii) Kusaidia kupokea wageni na kuwasaili shida zao, na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa
- (iii) Kusaidia kutunza taarifa/kumbukumbu za matukio, miadi, wageni, tarehe za vikao, safari za Mkuu wake na ratiba za kazi zingine zilizopangwa kutekelezwa katika ofisi anamofanyia kazi, na kumuarifu Mkuu wake kwa wakati unaohitajika.

- (iv) Kusaidi kutafuta na kumpatia Mkuu wake majalada, nyaraka au kitu chochote kinachohitajika katika shughuli za kazi hapo ofisini.
- (v) Kusaidia kufikisha maelekezo ya Mkuu wake wa kazi kwa wasaidizi wake na pia kumuarifu kuhusu taarifa zozote anazokuwa amepewa na wasidizi hao
- (vi) Kusaidia kupokea majalada, kuyagawa kwa Maofissa walio katika sehemu alipo, na kuayakusanya, kuyatunza na kurudisha sehemu zinazohusika.
- (vii) Kutekeleza kazi zozote atakazokuwa amepangiwa na Msimamzi wake wa kazi.

### **1.3 MSHAHARA:**

Cheo hiki kina ngazi ya mshahara wa – **TGS B.**

## **2.0 DEREVA DARAJA LA II – NAFASI MBILI (02)**

### **2.1 SIFA ZA MWOMBAJI**

Kuajiriwa wenye Elimu ya Kidato cha Nne (IV) au Sita (VI) aliyehitimu mafunzo ya udereva, awe na leseni Daraja 'E' au 'C1' ya uendeshaji magari ambayo amefanyika kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali. Awe amehudhuria mafunzo ya uendeshaji magari '*Basic Driving Course*' yanayotolewa na Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) au Chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali. Waombaji wenye cheti cha majaribio ya ufundi daraja la II watafikiriwa kwanza.

### **2.2 MAJUKUMU YA KAZI**

- (i) Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari
- (ii) Kupeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kazi
- (iii) Kufanya marekebisho madogo madogo ya gari

- (iv) Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali
- (v) Kujaza na kutunza taarifa zote za safari katika daftari la safari
- (vi) Kufanya usafi wa gari
- (vii) Kufanya kazi nyingine atakazoelekezwa na msimamizi wake.

### **2.3 MSHAHARA**

Cheo hiki kina ngazi ya mshahara wa – **TGS B.**



### 3.0 MASHARTI YA JUMLA KWA KAZI ZOTE

- i) Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania wenye umri kuanzia miaka 18 na wasiozidi umri wa miaka 45.
- ii) Waombaji wote wawe tayari kufanya kazi sehemu yoyote katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma
- iii) Waombaji wote waambatishe nakala ya cheti cha kuzaliwa, vyeti vya taaluma, Kidato cha Nne na cha Sita pamoja na vyeti vya mafunzo mbalimbali vinavyohusika.
- iv) Waombaji wote waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed CV) yenye anwani na namba za simu za kuaminika, pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.
- v) Picha tatu "Passport size" za hivi karibuni na ziandikwe jina kwa nyuma.
- vi) "Testimonials", "**Provisional results**", "**Statement of results**", Hati ya Matokeo ya Kidato cha nne "**result slip**" **havitakubaliwa**.
- vii) Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa tu kama wana Kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi
- viii) Waombaji wenye vyeti vya Kidato cha Nne na Cheti cha Taaluma ambao vimepatikana Nje ya Nchi wahakikishe vimehakikiwa na Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA) na Baraza la Elimu ya Ufundi (NACTE).
- ix) Watakaochaguliwa kufanya usaili watajulishwa tarehe ya usaili.
- x) Uwasilishaji wa taarifa za kugushi utaadhibiwa kisheria; aidha, maombi yote yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza na yanaweza kuwasilishwa moja kwa moja Ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma au kutumwa kupitia Posta kwa anuani ifuatayo:-

**Mkurugenzi wa Jiji,  
Halmashauri ya Jiji la Dodoma,  
1 Mtaa wa CDA,  
S.L.P. 1249,  
DODOMA.**

- xi) **Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 10 Juni, 2022  
Saa Tisa na nusu (9:30) Alasiri.**



**Joseph C. Mafuru  
MKURUGENZI WA JIJI  
DODOMA**

